MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
DAWASA
Dar es Salaam Water Supply & Sanitation Authority
ISO 9001:2015 Certified

# DAWASA YETU

TAREHE: 07 OKTOBA - 14 OCKOBA 2024 | TOLEO NA. 0178

# WAZIRI MKUU AIPONGEZA DAWASA KUCHAGIZA MATUMIZI NISHATI SAFI



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Kassim Majaliwa (Mb)** ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaaam (**DAWASA**) kwa kuchagiza agenda ya matumizi ya **Nishati safi ya kupikia** kupitia utekelezaji wa Mradi wa uchakataji topetaka (**Fecal Sludge Treatment Plant**) katika **Kata ya Somangila Wilayani Kigamboni**.

Ameeleza kuwa utekelezaji wa mradi huo utaleta manufaa ya matumizi ya nishati ya kupikia kwa **Wananchi** na **Wakazi** wa **Wilaya Kigamboni** na maeneo jirani.



"Niwatake **DAWASA** mshirikiane na **Sekta binafsi** katika kutoa huduma hii ikiwezekana kila Wilaya iwe na mradi kama huu wa mfanano ili **Wananchi** wetu wapate **Nishati safi** ya kupikia kama ambavyo Serikali ya awamu ya sita chini ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, **Dkt. Samia Suluhu Hassan** inasisitiza" alisema **Mhe. Majaliwa**.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu **DAWASA**, **Mhandisi Mkama Bwire** amesema utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 88** na ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha **nishati safi** ya gasi itakayotumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kupikia majumbani.

**DAWASA** inatekeleza miradi ya ujenzi wa mitambo ya kisasa ya kuchata topetaka katika maeneo ya **Wilaya za Kigamboni** (**Gezaulole, vijibweni na Golani**) na katika **Wilaya ya Ubungo** (**Kisopwa na Vikunai**) na **Wilaya ya Temeke** (**Vikunai**) yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 16.**